darasahuru.ac.tz

**HALMASHAURI YA WILAYA YA MKALAMA**
**MTIHANI WA MUHULA WA KWANZA**
**HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI**

**MUDA : MASAA 2:30** **26 MEI, 2025**

**MAELEKEZO**

1.Karatasi hii ina sehemu **A, B** na **C** zenye jumla ya maswali (10)
2. Jibu maswali yote katika sehemu **A**, **B** na **C**
3. Sehemu **A** na **C** zina jumla ya **alama (30)**, **alama 15** kwa kila sehemu na sehemu **B** ina alama (70)
4. Zingatia maelekezo ya kila sehemu na ya kila swali
5. Andika jina lako kwa usahihi upande wa kulia juu ya karatasi uliopewa

**SEHEMU A (Alama 15)**
**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

1. Katika kipengele (i) hadi ( x), chagua herufi ya jibu sahihi kisha andika herufi ya jibu hilo katika sehemu uliopewa.

i. Wakati wa masimulizi yake kuhusiana na jamii za asili za kitanzania, mzee Mponda alisikika kulitaja kundi moja na kusisitiza kuwa ndio kundi linaloaminika kuwa ni wazawa halisi wa iliyokuwa Tanganyika. Je kundi lipi kati ya haya yafuatayo?
A. Wakichembe B. . Wabantu C. Wakushito D. Wanilo. (. )

ii. Katika kuonesha kuwa somo la Historia ya Tanzania na maadili ni somo ambalo linauhusiano na masomo mengine, mwalinu Jamuhuri alitoa maelezo kuwa " husaidia kueneza, kuhifadhi na pia kuelezea maadili ya jamii" . Je uhusiano huu ni katika somo gani katika haya yafuatayo?
A. Kiswahili na Kiingereza B. Muziki C. Jiografia D. Hisabati. (. )

iii. Ni shughuli gani kuu ya kiuchumi ambazo jamii ya wakushito walijishughulisha zaidi katika maisha yao?
A. Kilimo, ufugaji na uvuvi B. Kuwinda, kukusanya matunda na kurina asali.
C. Kilimo na ufugaji D. Uvuvi, biashara na ufugaji. (. )

iv. Kila jamii ina miongozo yake ambayo hutawala tabia na matendo ya mtu mmojammoja au jamii kwa ujumla. Moja kati ya istilahi zifuatazo inaakisi miongozo hiyo:
A.Tabia B. Historia C. Urithi D. Maadili (. )

v. Fasihi, falsafa, ujuzi na lugha huweza kuwekwa katika kigawanyo kipi cha aina zifuatazo za Urithi?
A. Urithi wa kisanaa B. Urithi usioshikika C. Urithi wa asili D. Urithi unaoshikika. (. )

vi. Wanilo ni watu wa asili ya Bonde la Mto Naili ambao wanatumia lugha ya kinilo. Jamii hii iliingia Tanzania ikitokea:
A. Kameruni B. Ethiopia C. Kusini mwa Sudan D. Somalia. (. )

vii. Maadili ni kama kiumbe ambacho uimara na uhai wake hutegemea zaidi jitihada za mtu mmojammoja na jamii kwa ujumla ili yaweze kuwepo kwa matumizi ya muda mrefu. Je ni mifuno ipi ya kijamii kati ya hii ifuatayo ilisaidia katika ujenzi wa maadili Tanzania kabla ya ukoloni?
A. Dini na siasa B. Familia na mavazi

darasahuru.ac.tz

C. Kiuchumi na kijamii D. Jando na unyago. (. )
viii. Ni lipi kati ya haya yafuatayo ni chimbuko la jamii za asili ya watu wa pwani na Zanzibar?
A. Wanilo B. Waislamu C. Wabantu D. Wakushito. (. )
ix. Dhana ipi kati ya hizi zifuatazo inahusu mambo au matukio yaliyopita yenye athari kubwa kiuchumi kisiasa na kiutamadini?
A. Maadili B. Historia C. Urithi D. Utamaduni (. )
x. Jamii za kitanzania zinahimizwa sana kutunza na kuenzi maadili ya Taifa. Ni sababu ipi kati ya hizi zifuatazo inachagiza msisitizo huo?
A. Kupunguza uhalifu B. Kujenga tabia mbaya
C. Kukuza utalii D. Ni hifadhi ya Taifa. (. )

2. Oanisha vipengele vinavyoendana katika **Orodha A** na vile vya **Orodha B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi katika sehemu uliopewa.

| ORODHA A | ORODHA B |
|---|---|
| i. Jamii ni watu ambao ni wanaume, wanawake na familia zao | A. Ukoo |
| ii. Kundi la watu wanaozungumza lugha moja na huwa na mila na desturi za aina moja | B. Kabila |
| iii. Jamii ni mkusanyiko wa watu kwa ujumla wake | C. Jean Jacques Rousseau (1797) |
| iv. Kikundi kidogo cha watu wenye uhusiano wa damu au ndoa kinachoundwa na baba, mama, watoto na ndugu wengine. | D. John James |
| v. Jamii ni jumla ya watu mmoja mmoja | E. Margaret Thatcher (1987) |
| | F. Maadili |
| | G. Jamii za asili |
| | H. Emile Durkheim (1884) |
| | I. Familia |

MAJIBU

| ORODHA A | i | ii | iii | iv | v |
|---|---|---|---|---|---|
| ORODHA B | | | | | |

**SEHEMU B ( Alama 70)**

**Jibu maswali yote katika sehemu hii**

3. Bainisha matendo matano ( 5) ya kimaadili unayotenda au kutendewa ukiwa na wenzako maeneo ya shuleni au wazazi ukiwa nyumbani.
4. Kwa mtu ambae angependa kutunza Urithi wa jamii za kitanzania lakini anaonesha kukosa maarifa ya njia za kutunza urithi, unadhani ni njia zipi tano ambazo ungemshauri azitumie ili kutunza Urithi huo?
5. Unadhani ni kwa nini viongozi nchini wamekuwa mstari wa mbele kupinga vitendo vya rushwa? (**Toa hoja tano (5)**)
6. Jamii za asili ya kitanzania zilikuwa na Mila na desturi zilizolenga kukuza maadili katika nyanja mbalimbali za maisha yao. Fafanua kwa kifupi malengo matano (5)ya ujenzi wa maadili katika jamii hizo.

7. Jamii za asili ya kitanzania zimekuwa na historia ya muda mrefu ya kuwa na mifuno yao ya uendeshaji wa siasa zao kulingana na jamii husika. Bainisha sifa tano (5) zilizotumika kumpata kiongozi wa jamii za kibantu.
8. Ni kwa namna gani maadili yanaweza semwa kuwa yanatija kwa familia na Taifa kwa ujumla? (**Toa hoja tano (5) tu**)
9. Urithi wa kihistoria ni fursa kwa maendeleo binafsi na jamii kwa ujumla. Eleza kwa kutumia hoja tano ( 5) juu ya umuhimu wa urithi wa kihistoria wa jamii za kitanzania.

**SEHEMU C ( Alama 15)**
**Jibu swali la kumi 10**

10. Marafiki zaidi ya wawili wakiwa wamekaa pamoja wanajadiliana jinsi ya kukuza na kulinda maadili na urithi wa Tanzania. Lakini kikwazo kilichobainika ni kuwa wote hawajui ni nini wafanye ili kufanya maadili na urithi ukuwe na kulindika kwa matumizi ya kizazi cha sasa na kijacho. Kama ungepata fursa ya kuwa mshiriki wa mjadala huo, je ni matendo gani matano (5) ungeyabainisha kufanywa na kila mwanajamii ili kukuza na kulinda maadili na urithi wa Tanzania?